**Kilimo kinavyokausha vyanzo vya maji**

**Na Albano Midelo**



Vyanzo vingi vya maji katika mikoa mbalimbali nchini vimekauka kutokana na kuendekeza kilimo cha mabondeni hali iliyosababisha sasa vijito vingi mito iliyokuwa inatiririsha maji mwaka mzima kukauka.

Wilaya ya Mbinga Mkoa wa Ruvuma miaka 20 iliyopita kila bonde lilikuwa na maji ya kutosha,vyanzo vya maji vilikuwa vingi lakini sasa hivi ukitembea mabonde mengi maji yamekauka hali ya vyanzo vya maji ni mbaya**.**

Mkurugenzi Mhifadhi Mstaafu wa Wizara ya Maliasili na Utalii Ngwatura Ndunguru anabainisha kuwa siku za nyuma katika milima ya umatengo kulikuwa na mifereji mingi ambayo ilichimbwa na wananchi wa wilaya hiyo kwa ajili ya kujiletea maji jirani kwa matumizi ya umwagiliaji katika kilimo cha mabondeni au kiangazi ambapo hivi sasa vijito,mito na mifereji karibu yote imekauka na maji hakuna tena.

Anasema Wilaya ya Mbinga ipo milimani ambapo sehemu kubwa ya mito katika Mkoa wa Ruvuma inaanzia kwenye milima ya Umatengo na kwamba wilaya hiyo ndiyo inayoongoza kwa uharibifu mkubwa wa mazingira

unaotokana na shughuli za kibinadamu.

Changamoto za kimazingira ambazo zinaikabili Wilaya hiyo ni mahitaji makubwa ya ardhi ambayo yanatokana na idadi kubwa ya watu waliopo hali ambayo inawalazimisha kuvamia maeneo mengine ambayo hayastahili kisheria kama vile vyanzo vya maji na hifadhi za wanyamapori kama Liparamba hali ambayo inasababisha uharibifu mkubwa wa mazingira .

Kilimo cha mabondeni au kiangazi kinaleta athari kubwa za kimazingira kutokana na wananchi kulima hadi maeneo kingo ya mito ambayo hayastahili kulima kwa kuwa ni vyanzo vya maji hali hiyo inasababisha mito kukauka na kupotea.

Musa Mbunda ni Afisa Maliasili wa Kata ya Tingi anasema maeneo mengi katika Wilaya ya Mbinga vyanzo vyake vya maji vimeharibiwa kutoka na tabia ya wananchi kuachwa huru kutengeneza mifereji yao ya maji kutoka kwenye vyanzo vya maji kuunganisha maji na kwenda katika nyumba zao kwa ajili ya matumizi mbalimbali hali ambayo inasababisha mito kupoteza njia yake ya asili na kusababisha mmomonyoko wa udongo na vyanzo kukauka.

“Tatizo hili la wananchi kujitengenezea mifereji yao ni kubwa na linafanyika karibu katika vijiji vyote vilivyopo katika milima ya Umatengo Wilaya ya Mbinga hali ambayo hivi sasa imesababisha mabonde mengi ya maji na vyanzo vya maji kukauka,mito imepoteza uelekeo,wananchi wana tabia ya kutega maji na kumwagika nchi kavu huu ni uharibifu mkubwa wa mazingira ’’,anasisitiza.

Ndunguru anasema kilimo cha mabondeni au kwenye vyanzo vya maji ni kilimo cha kukausha maji hakifai kwa kuwa hivi sasa vyanzo vya maji vingi katika wilaya ya Mbinga vimekauka kutokana na kilimo hicho cha kiangazi.

“Mimi kijijini kwangu nimezuia kilimo hiki,serikali ndiyo iliyoruhusu kilimo cha mabondeni eti wananchi waongeze mapato matokeo yake sasa vyanzo vya maji vimekauka,mito na vijito vingi vya Mbinga vimekauka,kwa mfano ukanda wa chini wa kata za Mpepai vyanzo vya maji vimekauka na hivi sasa wananchi wanapata maji katika maeneo ya mbali na wanapoishi wakati zamani maji yalikuwa karibu na kwao’’,anasema.

Makamu wa Rais Mstaafu Dk.Mohamed Gharib Bilal anasema nchi inakabiliwa na uharibifu mkubwa wa vyanzo vya maji na ardhi,uharibifu ambao unatokana na shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kilimo kisicho cha hifadhi,ulimaji katika vyanzo vya maji,kwenye vilele, mitelemko mikali ya miinuko na milima pamoja na umwagiliaji usiokuwa endelevu.

Sababu nyingine alizitaja kuwa ukataji miti hovyo kwa ajili ya kuni na mkaa,uchomaji moto misitu na kwamba kutokana na uharibifu huo athari kubwa katika vyanzo vya maji zimeanza kujitokeza ambapo vina vya maji vimeanza kupungua kwenye mito,mabwawa,maziwa na kwamba hali hiyo ispodhibitiwa mapema mifumo ya mvua itabadilika,vyanzo vya maji vitakauka,uzalishaji wa mazao ya kilimo utapungua na nchi itakuwa kame.

Waziri Mkuu Mstaafu Mizengo Pinda anatoa rai kwa watanzania wote kutafakari iwapo kila mmoja amechukua hatua zinazostahili katika kuhifadhi mazingira ya nchi.

Hata hivyo kutokana na changamoto kubwa katika mazingira aliasa watanzania wote kuacha tabia ya kuharibu vyanzo vya maji, kufyeka miti ovyo na uchomaji misitu tabia ambazo alisema zinachangia kupoteza uoto wa asili badala yake alisisitiza upandaji na utunzaji miti ambazo ni moja ya hatua muhimu ya kuhifadhi mazingira.

“Mazingira ni sehemu ya maisha ya binadamu,na ndio uhai wa Taifa lolote,binadamu hawezi kuishi bila kutumia mazingira yanayomzunguka kwa mfano ardhi,misitu na mimea mbalimbali,maji na hewa,hata hivyo licha ya umuhimu huo tunaendelea kushuhudia uharibifu mkubwa wa mazingira katika nchi yetu hususan uharibifu wa misitu’’,anasisitiza Waziri Mkuu Mstaafu.

Sera ya Taifa ya mazingira kuhusu sekta ya maji katika kifungu namba 48 inaelekeza kulinda vyanzo vya maji na kudhibiti uchafuzi wa mazingira ambapo sera hiyo inaelekeza kuendeleza usimamizi bora wa maeneo chepechepe,upangaji na uendelezaji wa program za rasilimali za maji ili kulinda maeneo ya vyanzo vya maji na uoto wake na mimea.

Sera ya Taifa ya maji ya mwaka 2002 inalenga katika kuhakikisha kwamba vyanzo vya maji vilivyopo vinatunzwa,vinalindwa na kuendelezwa kwa

utaratibu unaozingatia uwiano wa mahitaji ya binadamu,mazingira na sekta nyingine za kiuchumi na kijamii,sera inaelekeza mkazo katika matumizi mazuri ya maji na kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji .

**Mwandishi wa makala haya anapatikana kwa baruapepe:albano.midelo@gmail.com,simu 0784765917**